



Imefadhiliwa na  
Umoja wa Ulaya

## VIUNGO

# Mradi wa Mtandao wa Thamani, Kilimo cha Bustani, na Ukuaji wa Mapato Zanzibar



VIUNGO inafungua uwezo wa mnyororo wa thamani wa kilimo cha bustani, inaongeza thamani na wingi wa bidhaa zenye ubora wa hali ya juu kwenye masoko, na inakuza ukuaji shirikishi wa uchumi Zanzibar.



## TAARIFA MUHIMU

**Sekta:** Kilimo (Bustani)

**Mshirika Kiongozi:** People's Development Forum (PDF)

**Washirika Wengine katika Utekelezaji:**

Community Forests Pemba (CFP), Tanzania Media Women Association (TAMWA) na Community Forests International (CFI)

**Bajeti:** EUR 5 005 449

**Mchango wa EU:** 4 500 000

**Muda wa Mradi:** 2020 - 2024

## USULI

Kilimo cha bustani ni mojawapo ya sekta ndogo zinazokua kwa kasi nchini Tanzania na imetawaliwa na wakulima wadogo. Sekta hii inatoa fursa za kuimarisha uchumi wa nchi huku ikiboresha moja kwa moja mapato ya wananchi wengi.

Licha ya maendeleo ya hivi karibuni, uzalishaji mdogo wa mazao ya kilimo kisiwani Zanzibar pamoja na kiwango kidogo cha lishe katika vyakula vinavyozalishwa humaanisha kuwa mahitaji ya lishe hayatoshelezi. Kadri ambavyo athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi zinavyozidi kudhoofisha kilimo cha bustani cha asili katika kisiwa hiki, ndivyo ukosefu wa usalama wa lishe unavyozidi kuongezeka. Kukosekana kwa usawa wa kijinsia pamoja na ukosefu wa uwezo wa kiuchumi wa wanawake huzuia kwa kiasi kikubwa haki ya uhuru ya wanawake na ustawi na ustahimilivu wa kisiwa hiki kwa ujumla.



## AGRI-CONNECT

Kusaidia Minyororo ya Thamani kwa Ustawi wa Pamoja katika Mazao ya Kahawa, Chai na Bustani

## MAELEZO YA MRADI

Mradi huu unakusudia kuongeza thamani na wingi wa bidhaa zenye ubora wa hali ya juu kwenye masoko kutoka kwa wakulima wadogo wa sekta ya kilimo cha bustani katika visiwa vya Unguja na Pemba. Shughuli za mradi wa VIUNGO pia zitaboresha upatikanaji wa vyakula vyenye virutubishi kwa kuwafundisha wakulima wadogo, haswa wanawake, kukuza mimea anuwai na ya thamani katika mifumo bunifu ya kilimo cha bustani ambayo inahimili mabadiliko ya tabianchi

### Shughuli kuu:

- Kuwakutanisha wahusika katika minyororo ya thamani na watunga sera ili kuboresha mifumo ya sera na ushirikiano.
- Kufundisha wakulima wadogo na maafisa ugani kuhusu Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi, Mbinu Nzuri za Kilimo,
- Usimamizi Jumuishi wa Wadudu na Magonjwa, na uhifadhi na utunzaji wa mazao baada ya kuvuna.
- Kutoa mitambo midogo na teknolojia inayofaa.
- Kuanzisha vituo vya usindikaji katika maeneo muhimu ambayo yanakuza miradi ya ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kilimo cha bustani.
- Kuwezesha mauzo, biashara na maendeleo ya kibiashara.
- Kusaidia Vyama vya Akiba na Mikopo vya Vijijini kujenga mahusiano na taasisi rasmi za kibenki na kuweza kufikia fedha za kuendeleza biashara.

## MATOKEO YATARAJIWAYO

### Ifikapo mwisho wa mradi, matokeo makuu manne yafuatayo yanatarajiwa kupatikana:

- Ushirikiano wa wadau mbalimbali kwenye ukuaji shirikishi wa uchumi katika sekta ndogo ya kilimo cha bustani umeongezeka.
- Uzalishaji katika kilimo cha bustani kinachohimili mabadiliko ya tabianchi umeongezeka.
- Chakula na usalama wa lishe wa wakulima wadogo wa kilimo cha bustani umeboreshwa.
- Uongezaji wa thamani katika kilimo cha bustani, mauzo, na biashara imeongezeka.

### Walengwa

Mradi utafikia walengwa 57,974 moja kwa moja na angalau asilimia 55 ya wanawake na wasichana na asilimia 33 ya vijana.

Kufanikisha matokeo katika mikoa inayokua katika visiwa vya Pemba na Unguja.

- ✓ asilimia 70 ya walengwa wanaboresha mapato yao
- ✓ Ongezeko la asilimia 35 katika thamani ya biashara ya ndani ya nchi
- ✓ Ongezeko la asilimia 20 katika thamani ya biashara ya kimataifa

## WASHIRIKA



COMMUNITY  
FORESTS  
INTERNATIONAL



COMMUNITY  
FORESTS  
PEMBA

**Solidaridad**

## MAWASILIANO

### People's Development Forum

Jengo la PDF, Sinza Mori, Nyuma ya Delina Apartments  
SLP 55021

Dar Es Salaam, Tanzania

Simu: +255 689 724 775:

Barua Pepe: info@pdftz.org:

Tovuti: www.pdftz.org



Imefadhiliwa na  
Umoja wa Ulaya

Email: [delegation-tanzania@eeas.europa.eu](mailto:delegation-tanzania@eeas.europa.eu)  
<https://www.eeas.europa.eu/delegations/tanzania>

EuropeanUnionTanzania  
 EUinTZ